

# AFYA YA UZAZI WA MAMA NA MTOTO
## TANZANIA

Japokuwa Tanzania imefanikiwa sana kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano, bado kupungua kwa vifo vya mama na watoto wachanga kumezorota. Kulingana na Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya wa 2015-16, takwimu za vifo vya mama zimeendelea kwa vifo 556 kwa kila wanawake 100,000 wanaojifungua kutokana na sababu kama ukosefu wa huduma bora, ukosefu wa huduma za dharura ya uzazi, uhaba mkubwa wa wanawake kuweza kupata huduma za afya kwa uhuru, na sababu zitokanazo na uzazi kama vile kutokwa na damu baada ya kujifungua. Vifo vya watoto wachanga, ambavyo ni asilimia 38 ya vifo vya watoto wote walio chini ya umri wa miaka mitano, vinabainisha umuhimu wa kushughulikia visababishi vikuu kama vile matatizo ya upumuaji, kuzaliwa njiti na maambukizi.

Miradi ya USAID ya Afya ya mama na mtoto (MCH) nchini Tanzania inaendelea kusaidia jitihada za kuzuia na kutokea Vifo vya Mtoto na vile vitokanavyo na Uzazi, ikitoa kipaumbele cha kuboresha afya ya wanawake walio katika mazingira magumu, wasichana, watoto wachanga, na watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Katika ngazi ya kitaifa, USAID inatoa usaidizi wa kitaalam kwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Tanzania bara na kuwezesha utoaji wa huduma za kuokoa maisha kwa akina mama, watoto wachanga, na watoto upande wa Zanzibar. Mifano ya usaidizi wa kitaalamu ni pamoja na kuandaa miongozo ya kliniki ya kujifungua kabla ya wakati, kutibu maambukizi kwa watoto wachanga, uanzishwaji wa chanjo mpya, na kuajiri wafanyakazi wa afya ya jamii. Hivi karibuni USAID imesaidia Wizara ya Afya kupanua na kutekeleza miongozo ya kitaifa ya kutoa huduma ya staha na heshima kwa jinsia na kwa afya ya uzazi jumuishi katika afya ya mama, watoto wachanga, na huduma ya afya kwa vijana nchini Tanzania. Mfumo huo huweka msingi wa mawasiliano bora, heshima na utu, na msaada wa kisaikolojia wakati wa kujifungua.

Jitihada za kuboresha utoaji wa huduma, zinaimarisha utoaji wa huduma bora kabla, wakati na baada ya kujifungua, ikishirikisha huduma zinazotolewa vituoni na kijamii katika kanda ya Magharibi na ya ziwa nchini Tanzania. Hii ni pamoja na:

## MUHTASARI WA MCH

### KIWANGO CHA UFADHILI

- Dola za Marekani Milioni 13 Mwaka wa Fedha 2020

### WASHIRIKA WAKUU

- Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
- Ofis ya Rais-Tawala za Miko ana serikali za Mitaa
- Wizara ya Afya-Zanzibar
- Jhpiego
- Deloitte
- fhi360
- Abt Associates
- PwC
- Vodafone Foundation
- Benki ya Dunia

### ENEO LA MRADI

Nchi Nzima, Kanda ya Ziwa na Magharibi

### MAWASILIANO

Laurel Fain – lfain@usaid.gov

o Kusaidia huduma jumuishi za ujauzito, huduma ya dharura ya uzazi wa mama na watoto wachanga, huduma ya msingi ya mtoto mchanga, unyonyeshaji pekee, na -huduma ya kangaroo njia inayotumika kuwahifadhi watoto wachanga wenye uzito wa chini inayohamasisha milo kidogo mara nyingi na kumuweka mtoto kwa kumkumbatia ngozi kwa ngozi; Upanuaji wa huduma baada ya kujifungua ni pamoja na kuanzishwa kwa huduma za uzazi wa mpango baada ya kujifungua ndani ya kipindi cha baada ya kujifungua;

o Kuanzisha mfumo thabiti wa ufuatiliaji na utoaji taarifa wa vifo vya mama na mtoto.

o Kuimarisha taaluma na uzoefu tiba wa wanafunzi katika miradi ya mafunzo ngazi ya uuguzi na ukunga ili kuhakikisha wanakuwa na ustadi pindi wanapohitimu.

## CHANGAMOTO

Changomoto ya rasilimali watu nchini Tanzania umesababisha upungufu wa watoa huduma katika vituo vya afya i. Katika kuongezeka kwa ugatuzi wa madaraka, uweo wa kujitegemeea ni fumbo la mipango mizuri ya halmashauri za wilaya ikiwa ni na kwa wakati katika kutekeleza ile miradi ya afya inayozorota.a. Wakati USAID imechangia katika kupunguza vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano, jitihada za kupunguza vifo ya mama na watoto wachanga imezorota, na kufikia kuvipunguza itahitaji kuimarisha mifumo inayoathira ubora wa huduma.

## MATOKEO

Tanzania imepiga hatua katika kukabiliana na vifo vya watoto kupitia chanjo, na mradi madhubuti wa kuzuia na kutibu malaria, na kuongeza uelewa, katika kukinga, na kutibu magonjwa ya mfumo wa hewa, magonjwa ya kuhara, na utapia mlo. Vifo hivyo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano vimeshuka kutoka vifo 166 mwaka 1990 hadi vifo 57 kati ya watoto 1,000 waliozaliwa hai mwaka 2017.

Kupitia ufadhili wa USAID mpango wa kitaifa wa chanjo umechangia kufanikisha uanzishwaji wa chanjo ya kuzuia magonjwa ya kuhara- a rotavirus, homa ya mapafu-pneumococcal, na surua / rubella. Kwa kushirikiana na Mpango wa Rais wa Marekani wa kuzuia Malaria, matibabu yameboreshwa kupitia utekelezaji wa matibabu jumuishi wa Programu ya Ugonjwa wa Watoto katika kanda ya Magharibi na ya Ziwa

Katika miaka mitano iliyopita, USAID imeendeleza uwekezaji katika kupunguza vifo vya akina mama na watoto wachanga kwa kuelekeza ufadhili wa kitaalam katika kuongeza upatikanaji na ubora wa huduma. Hivyo huduma zimeboreka sana katika maeneo ambayo USAID inatoa ufadhili:

| | |
|---|---|
| Asilimia ya kina mama waliopokea dawa za kukata damu kwenye mji wa mimba | **100%** |
| Asilimia ya watoto wachanga waliohuishwa wakati wa kuzaliwa | **72%** |
| Asilimia ya kina mama waliopata huduma baada ya kujifungua ndani ya siku mbili | **100%** |